

**Swahili transcript:**

Katika suala zima la kuondoa umaskini Tanzania, serikali imefanya mikakati mingi ya kuhakikisha kwamba umaskini unaondoka kama si kupungua katika nchi ya Tanzania. Aaah! Kama mnavyofahamu kwamba Tanzania ni mojawapo ya nchi zinazoendelea duniani. Lakini mpaka sasa serikali ya Tanzania imefanya mikakati mingi ya kuhakikisa kwamba umaskini unatokomezwa katika nchi hii ya Tanzania. Kwa hiyo kuna miradi mbalimbali ambayo serikali ya Tanzania pamoja na watu binafsi wameianzisha ili kuwawezesha watazania waweze kuondokana na hali ya umaskini. Nikizungumzia kuhusu miradi kwa mfano kuna asasi binafsi na asasi za kiserikali ambazo zinahusiana na suala zima la kuuondoa umaskini. Na asasi hizi zimewasaidia watazania walio wengi na mpaka vijijini zimefika ili kuweza kuwainua wananchi waweze kuwa wazalishaji mali na waweze kujikwamua katika hali ya maisha ya kila siku. Kwa hiyo kuna asasi ambazo zinahusika sana na jamii zimeanzisha shughuli mbalimbali za uzalishaji mali. Kwa mfano kuna asasi ambazo zinahusika na kuwaendeleza watoto wa kike ambao walikosa nafasi ya kwenda shule na wengine wakakaa nyumbani bila kufanya kitu chochote, na ambao walipata nafasi ya kwenda shule lakini wazazi wao walikuwa hawana pesa za kuwapeleka shule na hivyo kusababisha wale watoto kuendelea kukaa nyumbani. Asasi nyingine za watu binafsi zimefungua shule, kwa mfano shule za cherehani ili kuweza kuwawezesha hawa mabinti waweze kujipatia ujuzi wa kutengeneza au kushona nguo na hizo pesa ziweze kuwasaidia katika maisha yao, katika kumudu maisha yao ya kila siku, na hivyo kuendelea kuuondoa umaskini katika jamii. Kwa hiyo kuna mikakati mingi ambayo inaendelea mpaka sasa, kuna asasi za watu binafsi, asasi za kiserikali, na pia mataifa mengine duniani yamekuja Tanzania na yanaendesha shughuli mbalimbali ambazo zina lengo la kuwasaidia watazania waweze kujikwamua kutoka katika wimbi hili la umaskini. Kwa hiyo mpaka sasa Tanzania ipo katika hali nzuri na watazania wengi wamepata uelewa kwamba wanajua ni wajibu wao pia kujishughulisha ili waweze kuondokana na hali hii ya umaskini. Na wengi wamepata elimu, wengi wamepata mafunzo mbalimbali ya kuweza kuwasaidia hata kubuni miradi mbalimbali ya kufanya

kwa mfano kutengeneza batiki kama wakina mama, au kutengeneza na kuhifadhi vyakula na kuweza kuuza hata nchi za nje. Kwa hiyo kwa kufanya hivyo kumewasaidia pia wanawake hawa pamoja na watu wengine waweze kujikwamua katika hali ya umaskini na kuweza kujiongezea kipato katika familia zao.

**English translation:**

There are some strategies that have been put in place by the Tanzanian government to reduce, if not to remove, poverty in Tanzania. As you all know, Tanzania is one of the developing countries in the world, and the government is trying to make sure that poverty is being eradicated. There are projects which have been established by the government and private sectors to help people come out of poverty. These projects have been established even in rural areas to help people increase their daily income so as to have a good life. These projects work closely with the community with the main goal of improving the life of poor people.

One of the projects is one which deals with young women. This project aims to help young women and girls who didn't get a chance to go to school because their parents didn't have money to send them. As a result they stayed home doing nothing. Other private projects served to open vocational training schools to help these girls get skills such as tailoring. As they learn how to make clothes with sewing machines, the money they earn helps them manage their daily expenses. Apart from government and private projects which try to remove poverty, there are also international organizations which endeavor to help Tanzanians overcome poverty. At this point, Tanzania is in a good economic condition, and many Tanzanians understand that to live better, they need to work hard. Some of them have established small business like batiki making. Batiki is one of the Tanzanian cloths worn by all people regardless of age and gender. Women in particular cook and prepare food to be exported to other countries. Doing this helps these women and others eradicate poverty, increase their income, and have a good life.

**About CultureTalk:** CultureTalk is produced by the Five College Center for the Study of World Languages and housed on the LangMedia Website. The project provides students of language and culture

with samples of people talking about their lives in the languages they use everyday. The participants in CultureTalk interviews and discussions are of many different ages and walks of life. They are free to express themselves as they wish. The ideas and opinions presented here are those of the participants. Inclusion in CultureTalk does not represent endorsement of these ideas or opinions by the Five College Center for the Study of World Languages, Five Colleges, Incorporated, or any of its member institutions: Amherst College, Hampshire College, Mount Holyoke College, Smith College and the University of Massachusetts at Amherst.

© 2003-2008 Five College Center for the Study of World Languages and Five Colleges, Incorporated